# KIRUSI KIPYA CHA KORONA

## Unachohitaji kujua

Kirusi Kipya cha Korona (COVID-19) ni aina ya kirusi ambacho kinaweza kusababisha msururu wa magonjwa kwa binadamu kuanzia mafua ya kawaida hadi maambukizi makali ya njia ya kupumua kama niumonia. Kirusi kipya cha korona hakijawai kupatikana kwa binadamu hapo awali.

## Kinasambazwa vipi?



Kupitia kukohoa na kupiga chafya



Muingiliano wa karibu, kama vile kugusana na kusalimiana kwa mikono



Kugusa vitu au sehemu zilizo na virusi hivi, kisha kugusa mdomo wako, pua au macho kabla ya kuosha mikono yako



Watu ambao wamesafiri kuenda au kutoka Wuhan, China kuanzia Disemba 1, 2019, wanawezakuwa waathirika wa virusi hivi.Tafuta huduma za kimatibabu ikiwa ulisafiri kwenda Wuhan na ikiwa una homa, kukohoa au maambukizi ya kupumua, ndani ya siku 14 baada ya kurudi.

## Dalili zake ni zipi?



Homa



Kukohoa



Kupumua kwa shida



Maumivu makali ya ugonjwa

## Ikiwa ulisafiri kwenda Wuhan na unajisikia mgonjwa

- Baki nyumbani na ujizuie kugusana na wengine.
- Tafuta huduma ya matibabu mara moja. Kabla hujatoka kuenda kumuona daktari au chumba cha dharura, piga simu kimbele na ueleze kuhusu safari yako ya hivi majuzi na dalili za ugonjwa.
- Usisafiri ukiwa mgonjwa.
- Funika mdomo wako na pua kutumia karatasi ya tishu au sehemu ya mkono wa nguo yako (sio mikononi yako) wakati unakohoa au kupiga chafya. Tupa karatasi ya tishu kwenye jaa la taka.

https://www.orangecountync.gov/coronavirus

ORANGE COUNTY
HEALTH DEPARTMENT